Mkutano wa
UWABA
na
Wizara ya Miundombinu

14 January 2008

Yaliyomo

1) Utambulisho wa UWABA
2) Umuhimu wa baisikeli
3) Hali ya barabara za Dar es Salaam kwa wapanda baisikeli
4) Mapendekezo yetu
5) Vipi tunaweza kushirikiana kati ya UWABA na Wizara ya Miundombinu

1) Utambulisho wa UWABA

- Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
- Wanachama 153, wote wapanda baisikeli – za kawaida, za walemavu, maguta
- Tumeanzisha januari 2006

Utambulisho wa UWABA

Malengo yetu:

- Kushirikiana na serikali kutafuta mazingira mazuri na usalama kwa wapanda baisikeli Dar es Salaam
- Kufuatilia haki za wapanda baisikeli
- Kuelimisha wapanda baisikeli kuhusu matumizi mazuri ya barabara
- Kuhamasisha watu kupanda baisikeli

Mafanikiyo ya UWABA

- Tumesajiliwa na serikali januari 2006
- Tumefanya savei za barabara Temeke, Ilala na Kinondoni
- Tumekutana na TANROADS Dar es Salaam tarehe 24 Mei 2006 na makau makuu tarehe 27 septemba 2007, na tumewasiliana nao sana. Tumewasiliana na tumekutana na consultants za barabara.
- Tumepiga kampeni dhidi ya sera kupiga marufuku maguta kuingia maeneo ya jiji.
- Tumeandaa msafara mkubwa wa baisikeli tarehe 14 oktoba 2006 na tarehe 20 Oktoba 2007

2) Faida za baisikeli

- zinaondoa msongamano wa magari
- zinalinda mazingira na hazitoi moshi
- zinakuza uchumi wa nchi kwa kutotumia mafuta kutoka nje ya nchi
- Zina wezesha usafari wa bei nafuu na zinapunguza umasikini
- zinaboresha afya ya wapanda baisikeli na ya watu wengine kutokana na hewa safi

Umuhimu wa baisikeli

- Kupunguza msongamano wa magari
- Wanafunzi kufika shuleni mapema
- Kurahisisha watu kufika kazini na kufanya biashara
- Kurahisisha kusafirisha bidhaa
- Kurahisisha kuuza bidhaa (matunda, icecream)
- Watu wa siyojiweza - walemavu, wagonjwa, wazee
- Mazoezi na michezo

Umuhimu wa usalama kwa wapanda baisikeli

- 37% za safari za Dar es Salaam ni kwa miguu au baisikeli
- Mwaka 2006 wapanda baisikeli 30 walikufa na ajali Dar es Salaam, na 306 waliumia
- Tulipouliza kwa nini watu hawapandi baisikeli, 60% za majibu yalihusu usalama

Umuhimu wa usalama kwa wapanda baisikeli

Usalama unahusu

- Sheria na regulations za barabara
- Huduma za polisi
- Udereva wa magari
- Elimu ya wapanda baisikeli
- Miundombinu ambayo inalinda wapanda baisikeli

3) Hali ya barabara kwa wapanda baisikeli – barabara mbaya

- Kawawa Road, njia nyembamba hasa kutoka Kigogo mpaka Msimbazi upanda wa kushoto, na vituo vya dala dala
- Changombe, Kawe, Nelson Mandela, Barabara ya Kilwa, Sam Nujoma, Tegeta – hakuna njia za watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli

Hali ya barabara kwa wapanda baisikeli – barabara nzuri

Barabara ya Nyerere

- Kariakoo-Ilala njia nzuri sana upande mmoja
- Njia inapita nyuma ya kituo darajani - nzuri
- Njia ya baisikeli lami ni tofauti na eneo la watembea kwa miguu lakini hakuna alama

Barabara za Morogoro, Ali Hassan Mwinyi mjini-Morocco siyo mbaya sana lakini hakuna njia maalum kwa wapanda baisikeli

4) Mapendekezo yetu – barabara kubwa

- Kwenye barabara kubwa kawaida magari yanapita kwa haraka sana - ni hatari kwa wapanda baisikeli kuenda pamoja na magari
- Service Roads ni bora kuliko bila kuwa na service road lakini zina matatizo yake kama njia ya baisikeli:
  - Kama kuna watembea kwa miguu wengi, ngumu kwa baisikeli kupita, wanalazimishwa kushuka
  - Kwenye vituo vya mabasi ngumu kupita
  - Hatari kwa watembea kwa miguu hasa watoto kama kuna baisikeli zinazopita haraka
  - Hakuna alama au sheria kusema watu gani wapite wapi kwenye upande gani wa service road
  - Magari yanaruhusu kuingia service road, basi wanatumia kupaki na kupita foleni
  - Hakuna kitu cha kuziba magari kuingia service road

Mapendekezo yetu – barabara kubwa

- Pendekezo: Njia hasa kwa baisikeli, njia hasa kwa watembea kwa miguu, ambayo siyo service road kwa magari
- Sehemu maalum kwa wafanya biashara bila kuziba njia
- Sehemu maalum kwa fundi baisikeli
- Linda njia ya baisikeli kutoka magari – mfano karavat, kerbs, nguzo – epuka magari kuendesha na kupaki kwenye njia ya baisikeli
- Njia na nguzo ziwe pana za kutosha kwa guta, baisikeli za walemavu na kwa baisikeli kupitana
- Njiani uwezo wa kupita bila kushuka na kupanda tena (misingi njiani, mashimo makubwa, karavat njiani)
- Njia ipite nyuma ya vituo vya dala dala
- Alama kuonyesha njia ya baisikeli iko wapi
- Kama nafasi ipo, miti inayoleta kivuli bila kuziba njia

Mapendekezo yetu – barabara za kati kati

- Kwenye hizi barabara magari yasipite haraka
- Baisikeli zipite pamoja na magari, watembea kwa miguu wawe na footpath
- Tuta kupunguza mwendo wa magari
- Drainage kuepuka maji mengi njiani
- Shimo kubwa, uncovered drains, vitu vinavyo sababisha pancha ni hatari kwa wapanda baisikeli
- Mataa na reflectors
- Sehemu za kuvuka barabara kwa watembea kwa miguu na wapanda baisikeli mfano zebra ambayo ni tuta pia
- Daraja ziwe na nafasi kwa baisikeli na watembea kwa miguu

Mapendekezo yetu – sheria na regulations

- Nakala za sheria, regulations za barabara na highway codes zipatikani kwa urahisi kwa wananchi
- Wapanda baisikeli na wengine wanaotumia barabara tuwe na nafasi ya kuchangia mawazo yetu katika drafting ya sheria, regulations na codes
- Sheria ilinde haki na usalama wa wapanda baisikeli na watembea kwa miguu
- Alama za barabara zionyeshe wapanda baisikeli wapite wapi

Mapendekezo yetu - polisi

- Polisi watekeleze sheria
- Polisi wakamate wadereva wanaopaki kwenye njia za baisikeli au wanaotumia njia za baisikeli kupita foleni
- Wanaosababisha ajali wakamatwe, wapelekwe mahakamani na walipe fidia

5) Ushirikiano

UWABA tunapenda kushirikiana na Wizara ya Miundombinu. Tunaweza kuwasaidia:

- Kufanya savei za barabara
- Kutoa maoni wakati wa kupanga, kujenga na kurekebisha barabara
- Kutoa maoni wakati wa kuandaa sheria
- Kusaidia polisi kwa kutoa repoti ya wanaovunja sheria
- Kutoa feedback kuhusu hali za barabara
- Kuhamasisha watu kutumia barabara vizuri

Tunapenda kuwa na mawasiliano ya kila mara na Wizara tuwe na taarifa mapema ya mikutano n.k.